BARAZA LA MAASKOFU KATOLIKI TANZANIA

“NITAWEZAJE KUELEWA MTU ASIPONIONGOZA?” (Mdo 8:31)

UJUMBE WA KWARESIMA 2024

YALIYOMO

UTANGULIZI 4

SURA YA KWANZA 6

WONGOFU WA TOWASHI 6

1.1 Mahangaiko ya Towashi.....6

1.2 Hitaji la Kuongozwa.....8

1.3 Ujasiri na Unyenyekevu 10

SURA YA PILI 13

UMUHIMU WA NENO LA MUNGU.....13

2.1 Umuhimu wa kueleweshwa Neno la Mungu.....13

2.2 Mwana - JNNK na Neno la Mungu.....16

2.3 Namna ya Kusikiliza Neno la Mungu 17

2.4 Hitimisho 18

SURA YA TATU.....20

ATHARI ZA KUTOFAHAMU NENO LA MUNGU.....20

3.1. Kiimani 20

3.2 Kimaadili na ukosefu wa tunu za kiutu..... 21

3.3 Kiutamaduni 22

3.4 Kiuchumi.....23

3.5 Kisiasa 23

3.6 Uharibifu wa Mazingira 24

SURA YA NNE.....26

NINI KIFANYIKE?.....26

4.1 Kiroho 26

4.2 Kijamii 30

4.3 Kiuchumi 31

4.4 Kisiasa 33

HITIMISHO 36

UTANGULIZI

Kwa neema ya Mwenyezi Mungu tunaanza kipindi kingine cha Mwaka wa Kanisa, kipindi kitakatifu cha Kwaresima. Kwaresima inatupatia fursa ya kujitengenezea mazingira mazuri ya kuwa karibu na Mwenyezi Mungu. Ni kipindi cha siku arobaini ambazo kwazo msingi na maana yake inapatikana katika Maandiko Matakatifu.

Maandiko Matakatifu yanasema mtumishi wa Mungu Musa kwa siku arobaini alikuwa mlimani akimsikiliza Mwenyezi Mungu na kuandika. Katika kipindi hicho alifunga kula na kunywa (Mwanzo 34:28). Hii inatufundisha kuwa hizi siku arobaini zina mchango mkubwa katika kurekebisha maadili ya maisha yetu tukiongozwa na undani wa amri za Mungu na Maandiko Matakatifu.

Kwa siku hizi arobaini vilevile tunaalikwa kutembea na nabii Eliya aliyetembea siku arobaini akielekea Mlima Horeb akimtafuta Mwenyezi Mungu; na baada ya siku hizo akawa amempata (1 Wafalme 19:8). Mazingira magumu yaliyopelekea nabii Eliya atembee kwa siku zote hizo akimtafuta Bwana ni mazingira hayo hayo yanayotusukuma tutumie siku arobaini tukiwa tumejizatiti kumtafuta Bwana.

Hayo yote yanapata mwanga kamili toka kwa Mwalimu wetu Bwana wetu Yesu Kristo aliyefunga siku arobaini akijiandaa kuanza kazi ya kuhubiri Habari Njema ya wokovu kwa maneno na matendo makuu (Mt 4:1-11).

Kipindi hiki kinatupa fursa ya kutafakari kwa karibu mateso ya Kristo ikiwa ni njia ya kutukomboa toka utumwa wa dhambi. Ndani ya siku hizi arobaini tunatafuta nguvu za kuishi maisha yetu kama Wakristo imara wenye kulinda, kuthamini na kuishi ahadi zetu za ubatizo. Huo ndiyo ushindi wa ufufuko tunaotukuza na kuadhimisha siku ya Pasaka. Kupitia Ujumbe wetu wa Kwaresima, tunaalikwa tumwombe Mungu atupe uelewa wa Kimungu.

Towashi anayeongelewa katika ujumbe huu, alikuwa anatembea na uelewa wa kibinadamu kuelekea Yerusalemu kila mara kwenye ibada na kutoa sadaka, lakini hakuwa na uelewa wa Kimungu. Mara alipokutana na Filipo aliyekuwa na uelewa wa Kimungu ndipo na yeye akaweza kupata uelewa wa Maandiko Matakatifu. Kuna vitu vingi ambavyo usipovielewa vinakujengea mashaka na kukuletea mateso.

Tuombe kujaliwa uelewa wa Kimungu katika kila jambo. Tunahitaji uelewa wa Kimungu kwenye mambo ya kiroho, kiimani, kiuchumi, kisiasa, na kimaadili. Ukijikita katika uelewa wa kibinadamu pekee ndipo unaangamia katika njia ya upotevu. Sharti Mungu akubariki, akutunze na akupe neema ya kuwa na uelewa wa Kimungu.

Katika Kwaresima hii tunaalikwa kutafakari hali zetu za maisha, hasa Ukristo wetu mintarafu uhusiano wetu na Mwenyezi Mungu tukiongozwa na simulizi linalomhusu Filipo na Towashi. Hivyo tunatafuta kujua upendo na huruma ya Mungu kupitia Kristo aliye ufunuo kamili wa Mwenyezi Mungu.

SURA YA KWANZA

WONGOFU WA TOWASHI

Sura hii ya kwanza inaonesha mahangaiko ya Towashi. Mtumishi huyu wa Malkia wa Kushi (Ethiopia) aitwaye Kandake, alikuwa akitoka hija Yerusalamu. Akiwa katika gari lake alikuwa anasoma Neno la Mungu kwa nia ya **kuelewa na kupata wokovu**. Katika jitihada zake binafsi alishindwa kufikia lengo lake, alihitaji msaada wa mtu mwingine. Shemasi Filipo alifanikiwa kumwongoza Towashi hadi kuweza kutoka katika hali yake ya upagani na kubatizwa kwa sababu alikuwa mtu sahihi. Tunahitaji watu sahihi wa kutuongoza tuweze kuelewa Neno la Mungu vizuri na kuweza kupata wokovu.

1.1 **Mahangaiko ya Towashi**

Ukiwa umepoteza ufunguo wa nyumba au chumba na huna wa akiba, njia inayobaki ni kuvunja tu mlango ili uweze kuingia ndani. Kwa huyu Towashi wa Ethiopia ni kama mlango wake wa imani ulikuwa umefungwa na hakuweza kuingia na kuona. Alihitaji mtu wa kuvunja huo mlango ili aweze kuingia. Filipo mtume alifanya hiyo kazi ya kuvunja huo mlango ili Towashi aweze kuingia ndani mwake.

Kitabu cha Matendo ya Mitume, kinaelezea jinsi Towashi kutoka Ethiopia, ambaye alikuwa mwanafunzi wa dini ya kiyahudi alivyosaidiwa kuelewa Neno la Mungu na kisha kubatizwa. Alikuwa ametoka Yerusalemu kuhiji na kumwabudu Mungu wa Israeli. Alipata wongofu wake siyo kule Yerusalemu alikoenda kuhiji, ambapo

kulikuwa na mitume kama vile Petro na Yohani, ila jangwani alipokutana na shemasi Filipo. Filipo anatumika kama chombo cha Towashi huyo kuiona imani ya kweli. Mlango unaweza kuvunjwa popote si mahali ambapo tunategemea kama Yerusalemu, kanisani, nk; ila kama ilivyokuwa kwa Towashi hii inaweza kutokea popote na kusaidiwa na mmoja mwenye mang'amuzi kama Filipo.

Mungu mwenyewe ndiye anayetupatia wokovu. Ndiye yeye anayechagua wakati wa kufaa kwa kila mmoja wetu. Pale inapobidi, inaonekana ni yeye pia anachagua mtu wa kutuongoza au kuvunja kizuizi au mlango na kupanda mbegu ya imani ndani mwetu.

Filipo ni mmoja wa mashemasi saba waliochaguliwa baada ya kushuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho Mtakatifu na hekima ili waweze kuwahudumia wajane wa Kiyunani (rej. Mdo 6:1-6). Hii ilikuwa kuwapa mitume nafasi nzuri ya kusali na kuhubiri. Kisha shemasi Filipo ndiye aliyechaguliwa kumwongoza kwenye imani huyu mtumishi wa Malkia Kandake kutoka Ethiopia.

Towashi anaonesha mahangaiko yake ya imani. Anaonesha nia ya kufika sehemu fulani kiroho lakini peke yake hafaulu. Pamoja na safari ya mbali kutoka Ethiopia mpaka Yerusalemu na bidii yake kusoma Maandiko Matakatifu, lakini pekee yake hakufikia mahali alipotakiwa kuwa kiimani. Mahangaiko haya si ya Towashi tu, bali yanatupata hata sisi waamini wa nyakati hizi. Inabidi tuoneshe juhudi kama ya Towashi, pengine si ya kwenda mpaka Yerusalemu ingawa hiyo haiondolewi kwa anayeweza kuhiji. Juhudi ya kusoma Neno la Mungu, kusali, kushiriki Sakramenti hasa ya Upatanisho na Ekaristi Takatifu ni njia muhimu ya kuelekea wongofu.

Kipindi cha Kwaresima ni kipindi cha sala, kufunga na matendo ya huruma. Kwaresima kwa kawaida inajengwa katika nguzo hizo tatu. Matendo hayo na tafakari zingine ziweze kutugusa na kama Towashi nijiulize nini kinanizuia nisiende kuungama, kubariki ndoa yangu au kubatizwa?

1.2 Hitaji la Kuongozwa

Inaonekana ni muhimu sana mmoja kuongozwa ili kufikia wongofu. Hapa tunaona kwamba, Towashi licha ya kwenda Yerusalemu kuhiji na pengine kusoma aya hiyo au nyingine lakini hakufaulu kufikia ile hali ya wongofu. Yeye binafsi alijitahidi lakini hakufikia ile hali ya kuomba ubatizo na kama anavyoonesha kwenye maneno yake mwenyewe; "… nitawezaje kuelewa mtu asiponiongoza?" (Mdo 8:31).

Kwetu sisi kuna makundi mawili: watu walio tayari kuongozwa ili kupata wongofu na kundi jingine wasio tayari kuongozwa. Wale walio tayari kuongozwa, ni wale ambao wanafuata maagizo ya Mungu, Kanisa na ya viongozi mbalimbali walio halali. Wale ambao hawapendi kuongozwa, kuelekezwa, kuambiwa au kukumbushwa kitu ni wale ambao wanaona kuwa wanaelewa kila kitu. Kwa bahati mbaya tuko katika jamii ambayo walio wengi wanaona wanaelewa kila kitu. Wengi huona kuwa hawana haja ya mtu awasaidie maana wanafahamu kila kitu, wanaelewa watapata wapi majibu ya maswali yao.

Kuna sababu nyingi kwa nini watu hawapendi kuongozwa, tukitaja tu kwa uchache: mosi, tumeharibu na tunaendelea kuharibu mfumo wa familia. Familia nyingi siyo imara tena kuwa shule ya imani, maadili, matumaini na mapendo. Si tena kanisa dogo kwa watoto kujifunza kumjua na

kumpenda Mungu. Si tena shule ya sala. Matokeo yake ni kwamba watoto wengi hawamwoni kiongozi wa kweli. Mtoto hakumbuki kumwona baba au mama akimkemea na kumrekebisha kwa jambo baya na kumpongeza kwa mema afanyayo, au hata kumwambia ufanye hivi au usifanye vile, nk.

Pengine watu hawapendi kuongozwa kwa sababu baadhi ya viongozi wamepoteza ile hali ya kuwa viongozi bora. Kwa hiyo hawana tena mamlaka ya kumkumbusha mtu kitu cha kufanya kwa sababu wao wenyewe wanashindwa. Baadhi ya viongozi tumepoteza ule ujasiri wa kuondoa kwanza boriti lililo kwenye jicho letu ili tuweze kuwasaidia wengine kuondoa kibanzi kilicho kwenye jicho lao (rej. Mt 7:5). Badala yake tumeshindwa kuona kwa sababu macho yetu yana boriti lakini pia hatuna ujasiri kwani tutakumbushwa makosa yetu.

Tatizo la malezi si la familia tu. Taasisi zingine ikiwemo Kanisa hatufanyi ya kutosha katika malezi ya vijana na watoto. Idadi kubwa ya waamini wa Kanisa letu ni vijana na watoto, makundi haya yanafikia asilimia 75. Lakini ukiangalia hatuna utume wa pekee kwa vijana na watoto. Kama misa ya watoto, vijana au semina kwa ajili yao.

Hata katika Kanisa, wakati mwingine inakuwa vigumu kupata viongozi wazuri wenye sifa stahiki. Kuanzia kwenye Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo (JNNK) na sehemu zingine tumeendelea kuahirisha uchaguzi kwa sababu tumeshindwa kupata watu wenye sifa stahiki. Tunaposhindwa kupata viongozi wenye sifa nini kinatokea? Viongozi watatengenezwa ili wawe na sifa ya viongozi ingawa kimsingi hawana sifa hizo. Ndiyo maana tunaona makundi yakipita hapa na pale wakitumia nguvu nyingi

wakati mwingine hata za fedha ili tu yule wanayemfikiria apite. Watu wataaminishwa kwa namna na mbinu zozote kuwa huyu ni kiongozi na ana uwezo wa kufanya haya au alishawahi kuyafanya mahali pengine wakati hana hizo sifa.

Kwaresima hii itukumbushe nini tufanye kama Kanisa katika malezi ya vijana na watoto. Mapadre na watawa tuwe wa kwanza kutimiza wajibu wetu wa kuongoza kwa mifano ya maisha yetu. Pale inapobidi kupaza sauti ya kinabii tuipaze. Kila mbatizwa ni kuhani, nabii na mfalme (kiongozi). Tumebatizwa na tumetumwa ili kutangaza Neno la Mungu. Huku ndiko kutoana kutoka maisha ya dhambi na kupelekana kwa Mungu. Kila mmoja wetu anie kutekeleza wajibu huo muhimu.

1.3 Ujasiri na Unyenyekevu

Yote mawili, kuongoza na kuongozwa, yanahitaji ujasiri na unyenyekevu. Ni muhimu kuongozwa pale ambapo hatujui. Kama Towashi asingeongozwa asingepata wongofu na hatimaye ubatizo. Kiongozi yeyote anapaswa kuwa jasiri na aweze kukabili tatizo, kama ilivyo kuwa kwa Filipo. Kwa ujasiri anamwendea Towashi na kumwuliza, "Je unaelewa hayo unayosoma?" (Mdo 8:30). Alipojibu, la, Filipo alimwelewesha maana ya maneno hayo ambayo aliyasoma mara nyingi bila kuyaelewa. Aidha, awe na unyenyekevu wa kufanya yote kwa upendo na hivyo kukubalika na yule anayemwongoza. Wote wawili wanastahili pongezi. Kwa upande mmoja Filipo kwa ujasiri wa kwenda kumwuliza na kwa upande mwingine Towashi kwa unyenyekevu wake wa kukiri mapungufu yake na kukubali kuongozwa.

Viongozi waige mfano wa Filipo wa kufuatilia watu wao na kujua wanaweza nini na hawawezi nini. Wawe na huruma kwa watu wao na wawe tayari kuwasaidia kadiri wawezavyo. Waongozwa, nao wawe wanyenyekevu wa kusikia na kutii sauti ya viongozi wao, wawe na ujasiri wa kuuliza, kukubali kukosolewa, kusahihishwa na kurekebishwa.

Mtakatifu Paulo anapomwandikia Timoteo, Askofu, anamhimiza, "lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho" (2 Tim 4:2) anataka kuonesha nafasi ya Neno la Mungu katika kuongoza maisha ya waamini. Anasema, "kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kwa kuwaongoza na kwa kuwaadibisha katika haki" (2 Tim3:16). Wachungaji wajibidishe kuhubiri Neno hilo linalotuongoza katika kweli yote.

Neno la Mungu linatufundisha tuwe na ujasiri na unyenyekevu, si tu kama wa Towashi aliyeomba kubatizwa baada ya kuona maji yule Towashi akasema; "Tazama maji haya; ni nini kinanizuia nisibatizwe?" (Mdo 8:36); bali pia ujasiri na unyenyekevu kama ule wa Mwana mpotevu ambaye baada ya kutafakari sana, aliamua, nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kukiri makosa yangu. (rej. Lk 15:18). Tathmini ya kweli inayoongozwa na Neno la Mungu inachunguza dhamiri bila ya kujihurumia na kutoa majibu sahihi ya kumrudia Mungu. Itasaidia kutoa uamuzi wa kubadilisha mtindo wa maisha kwa kuacha maelekeo ya dhambi kwenda yale yanayomfurahisha Mungu. Ujasiri utanisaidia kubainisha makosa yangu na kwa unyenyekevu kuchukua hatua za kumrudia Mungu.

Kwaresima ni kipindi cha neema – kipindi cha kusali, kufunga na kufanya matendo mema. Katika Kwaresima hii tuombe kuwa na ujasiri wa kufunga (kwa wale wanaoweza) na kuongeza bidii ya kusali. Tena tusome kwa bidii Neno la Mungu na kulitafakari. Tuache dhambi na yote yanayomuudhi Mungu (rej. Mdo 9:4). Tuondoe vizuizi vyote vinavyotufanya tusipokee sakramenti za Kanisa. Kwa wale wasio na vizuizi, wajibidishe kupokea mara kwa mara Sakramenti ya Upatanisho na ya Ekaristi takatifu. Tuwapeleke watoto wetu kupokea Sakramenti za Ubatizo na Kipaimara na tuwahimize vijana wetu wafunge Ndoa takatifu. Tuwaombee wagonjwa na wazee wetu waweze kupata sakramenti za Kanisa. Kwa jinsi hii nasi tutapata wongofu ufundishwao na Kanisa kama ule alioupata Towashi.

SURA YA PILI

UMUHIMU WA NENO LA MUNGU

Towashi anatufundisha kupenda kusoma Neno la Mungu. Aliposhindwa kulielewa aliomba msaada – *nitawezaje kuelewa mtu asiponiongoza.* Mfalme Daudi alieleza kuwa Neno la Mungu ni taa ya miguu yetu kutuongoza kwa Mungu (rej. Zab. 119:105, Mit 6:23). Neno la Mungu linatuwezesha kujua sheria za Mungu na kuzishika. Kwa kulitii Neno la Mungu tunakuwa wanafamilia ya Mungu maana kila asikiaye Neno la kulifanya, ni ndugu ya Kristo.

2.1 Umuhimu wa kueleweshwa Neno la Mungu

Towashi anatuonesha kuwa kusoma Neno la Mungu ni jambo moja na kuelewa ni jambo jingine. Japo alipenda kulisoma, alihitaji mtu amfafanulie na amwongoze ili alifahamu kikamilifu na aweze kupata wokovu.

Kwa msaada wa Roho Mtakatifu, Shemasi Filipo anaongozwa kumkaribia na kumsaidia kulielewa Neno la Mungu. Shemasi Filipo analiwakilisha **Kanisa** ambalo lina wajibu wa kuongoza waamini kulielewa Neno la Mungu na kuliishi.

Bwana wetu Yesu Kristo aliyetumwa na Baba kuja kutukomboa, alishuka toka mbinguni kwa ajili yetu sisi wanadamu na kwa ajili ya wokovu wetu (rej. Kanuni ya Imani). Kwa umwilisho wake, Kristo aliunganisha Mbingu na dunia. Alitumia "muda" na "mahali" (dunia) kwani alisali, alifundisha, aliponya wagonjwa, alifufua wafu na

kuwahimiza watu kutubu na kuliamini Neno la Mungu. Sasa dunia ni mahali pa kumwona Mungu na kupata wokovu.

Kwa kuwatuma wafuasi wake waende duniani kote ili kuwafanya watu wote kuwa wanafunzi wake (rej. Mt. 28:16-20), na kwa kuwapelekea Roho Mtakatifu, alianzisha **Kanisa** ambalo litaendeleza kazi ya ukombozi aliyokuja kuifanya Yeye mwenyewe. Hivyo utume wa Kanisa ni ule ule ambao Kristo alikuja kuufanya hapa duniani.

Kabla ya ujio wa Kristo, Mungu aliongea na watu wake kwa njia mbali mbali bali sasa anaongea nasi kwa njia ya Mwanae Yesu Kristo (rej. Ebr. 1:2). Mungu mwenyewe alimtambulisha kwetu Kristo kwa kusema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, msikieni yeye" (Mk. 9:7). Huyo mwana mpendwa naye aliweka wazi kuwa "Kwa maana mtu ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Mungu, huyo ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu" (Mk. 3:35). Hivyo, wote wanaolisikia Neno la Mungu na kulitii ni wanafamilia ya Mungu na wana-Kanisa.

Kwa njia ya Kanisa tunaelewa kwamba, Neno la Mungu:

- Ndilo linalotujengea **imani ya kweli** (rej. Ebr 11.1k). Imani hiyo hutokana na kusikia Neno la Mungu (rej. Rom. 10:17). Imani ya kweli ndio inayotusaidia kutenda matendo mema yampendezayo Mungu na kuacha mabaya. Ni sauti ya Mungu inayotufundisha, kutuonya, kutuongoza katika njia sahihi na kutuadibisha katika haki.
- Hutuepusha na dhambi na kutufanya wenye moyo safi (Zab.119:11, Yn 15:3)

- Linaponya. Kwa njia ya Neno lake, Kristo aliwaponya wengi waliokuwa dhaifu kimwili na kiroho (Mt. 8:7, 13; Mk. 2:9-12; Mdo 14:8-10). Hutuletea uzima wa sasa na wa milele. Kristo alisema, anayeniamini, hata kama amekufa, ataishi; na kila anayeishi na kuniamini, hatakufa kamwe (rej. Yn. 11:25-26). Aidha linatusaidia kumtambua Kristo. (Lk 24:45).

- Ndilo kweli (Yn 17:17) na tena ni silaha, ni upanga wa roho (Efe 6:17).

Kanisa linatualika kuendelea kuenzi yale yanayoelekezwa juu ya Neno la Mungu na Mamlaka fundishi ya Kanisa (Magisterium). Kwa mfano:

- Vilipotokea vikundi mbali mbali vya watu waliotaka kutafsiri Biblia kwa kutumia akili binafsi (rationalism and higher critics) au kutumia sayansi ya kidunia (physical science), Baba Mtakatifu Leo aliandika *ensiklika* iitwayo *Providentissimus Deus*, akikemea kuwa Biblia ni kitabu cha imani, kilichoandikwa kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu. Lazima kiheshimiwe.

- Tarehe 15 Septemba 1920, Baba Mtakatifu Benedikto XV, alitoa *ensiklika* iitwayo *Spiritus Paraclitus*, akisisitiza kusoma Neno la Mungu kwa mwanga wa Roho Mtakatifu.

- Mtaguso Mkuu wa Pili wa Vatikani katika hati yake ya kidogma iitwayo *Dei Verbum*, ukisisitiza tafsiri na

uelewa wa Biblia katika maagano yote mawili, yaani Agano la Kale na Jipya, pia uliwataka wataalamu wa kikatoliki wa Biblia, wakifuata mwongozo wa Kanisa, wajifaidishe na kuendeleza michango yote ya wafafanuzi wa Neno la Mungu waliotangulia, kwa namna ya pekee mababa watakatifu na walimu wa Kanisa, kuhusiana na kuelewa Neno la Mungu.

- Kwa kuenzi umuhimu wa Neno la Mungu, Baba Mtakatifu Fransisko kupitia *motto proprio* iitwayo *Aperuit illis*, aliaagiza kuwa kila Dominika ya tatu ya Mwaka, ni Dominika ya Neno la Mungu.

Hayo yote yametajwa ili kuonesha umuhimu wa Neno la Mungu kwa maisha na wokovu wa mwanadamu. Mtakatifu Yeronimo alisema kuwa kutojua Maandiko Matakatifu ni kutomjua Kristo.

2.2 Mwana - JNNK na Neno la Mungu

Kwanza kabisa ni vyema tutambue kuwa ukristo ni wito wa kumfuasa Kristo. Wito huu ni wito wa kuwa mtakatifu. Mwanajumuiya wa JNNK kwa namna ya pekee anaitwa kuuishi wito huu wa kuwa msikivu kwa Neno la Kristo anayemfuasa kama kondoo alivyo msikivu kwa sauti ya mchungaji wake; "Kondoo wangu huisikia sauti yangu; mimi nawajua, nao hunifuata" (Yohane 10:27).

Mwanajumuiya wa JNNK msikivu kwa sauti ya Kristo ni mkristo mwaminifu katika ufuasi wake na katika kuuishi wito wake wa ukristo. Ni mtu anayetamani utakatifu. Mkristo anayeishi kweli wito wake ni kondoo mwaminifu wa

Kristo. Mwanajumuiya wa JNNK anao wito mmoja msingi, ambao ni kuisikiliza sauti ya Kristo ambayo ndilo Neno la Mungu na kulifanya kuwa ni taa na dira ya maisha yake. Afanyaye hivyo kwa uaminifu huwa mwana mpendwa wa Mungu pamoja na Kristo anayemfuasa. Kuisikiliza sauti ya Kristo yaani Neno la Mungu ni amri ya Mungu. Katika tukio la kugeuka sura Mungu anasema "…huyu ni mwanangu mpendwa msikilizeni yeye" (Mk 9:7). Mwanajumuiya kama mfuasi wa Kristo hawezi kuepa agizo hili la Mungu Baba na akaendelea kuwa mkristo mkamilifu. Kumsikiliza Kristo ni kulisoma Neno lake, kulifahamu na kuliweka katika matendo yaani kulifanya kuwa sehemu muhimu ya maisha ya Mkristo likimwangazia katika safari yake ya kwenda mbinguni.

2.3 Namna ya Kusikiliza Neno la Mungu

Wanajumuiya wa JNNK kama watoto wa Mungu na ndugu zake Kristo, tulisikilizeje Neno la Mungu Baba yetu ili tupate kuwa wana wapendwa wa Mungu? Tukirejea katika Maandiko Matakatifu tunatambua kuwa dhana ya kumsikiliza Muumba wetu inahitaji nidhamu ya hali ya juu inayodai kuyatiisha maumbile yetu yote. Sehemu ya injili ya Marko (Mk 12:28-34) ambayo kimsingi hutoka katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati 6:4 – 9, inatufundisha jinsi ya kulisikiliza na kuliishi Neno la Mungu. Kusikiliza Neno la Mungu kunapashwa kufanywa kwa nidhamu ya hali ya juu kama mtoto mwenye adabu na heshima anavyotakiwa kuenenda mbele ya wazazi wake.

2.4 Hitimisho

Ikumbukwe kuwa si kila mtu anaweza kuwa mwalimu wetu. Ukweli ni kwamba tunaweza kujifunza kitu fulani toka kwa kila mtu, kila mmoja ana kitu cha kutufundisha, lakini si kila mmoja anaweza kutufundisha katika mambo yahusuyo imani na maadili. Kwa upande wa imani na maadili ya kikristo kunahitajika Roho wa Bwana anayefanya kazi kupitia watu waliochaguliwa na kuidhiniswa rasmi mfano wa Filipo.

Kanisa Katoliki liko makini sana katika kuchagua na kufuatilia wahudumu wa Neno la Mungu wanaohusika kutoa mafundisho ya imani na maadili. Kupitia Mtaguso Mkuu wa Pili wa Vatikano na mitaguso mingine iliyotangulia, Kanisa Katoliki linaweka wazi msimamo wake wa ni nani walio na madaraka ya kufundisha Neno la Mungu. Kuna hiarakia ya wale wanaoweza kufundisha kwa niaba ya Kristo na Kanisa (mashemasi, mapadre, maaskofu) na waamini wengine waliojaliwa kuwa mashahidi wa Kristo waliopewa tunu ya ufahamu wa imani thabiti na wenye mvuto katika kuongea.[1]

[1] Hati ya Mtaguzo wa Pili juu ya Kanisa, *Lumen Gentium*, 1964, namba 3

Pamoja na wahudumu hao, Kanisa linafuatilia maudhui na kile chote kinachofundishwa. Hili linafanyika ili kulinda kundi walilokabidhiwa lisipotee kwa kujua kuwa yapo mafundisho potovu. Maandiko Matakatifu yanatuasa na yanatuonya kuhusu mafundisho potovu. Mtakatifu Yohana anapoandika analiweka jambo hilo wazi:

> *Wapenzi, msiiamini kila roho, bali zija- ribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu kwa sab¨bu manabii wa uongo wengi wametokea duniani,* (1Yn 4,1).

Aya hii imebeba unabii wenye ukweli ulio wazi katika jambo hilo. Haya ndiyo yanayotokea katika enzi zetu hizi. Manabii wa uongo wanajitokeza kila kukicha. Mbaya zaidi baadhi ya Wakatoliki wenzetu wanafuata mafundisho hayo potovu. Mafundisho yaliyojaa udandanyifu wa wazi, wakiahidiwa uponyaji, utajiri, vyeo, wakifuata eti bahati. Wanasahau imani, maadili yao na kanuni halisi za kupata hayo. Matokeo yake ni kudanganywa tu.

SURA YA TATU

ATHARI ZA KUTOFAHAMU NENO LA MUNGU

Tunakubaliana na Nabii Hosea pale anaposema ***"Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa …"*** **(Hos. 4:6).** Watu wengi wamepata madhara makubwa ya kimwili na kiroho; wameangamia na wengine wameangamiza watu kwa sababu ya kukosa maarifa. Madhara mengi yanayotokea kila uchao yanatokana na kutokuelewa au kutokueleweshwa kwa kina juu ya Neno la Mungu. Madhara haya yaweza kuwa ya kiimani/kiroho, kimaadili/kiutu, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kimazingira, kutaja lakini kwa uchache.

3.1. Kiimani

Mtakatifu Anselm, mtawa, mwanateolojia, na Askofu Mkuu wa Canterbury, aliamini kwamba imani inahitajika katika kufahamu, lakini pia akili ni muhimu katika kuelewa. Kulingana na Anselm, imani ya kikristo huanzisha jitihada ya kumjua na kumuelewa Mungu na kile tunachokiamini kumhusu yeye (rej. Ebr. 11). Imani, kulingana na Anselm, inawafanya waamini kutafuta ufahamu kwa furaha ya kumjua Mungu na kumpenda.

Ukosefu wa ufahamu wa kina wa Neno la Mungu umekuwa kisababishi kikuu cha "afya mbaya Kiroho." Watu waliolegea kiimani badala ya kutafuta huduma stahiki (kwa mfano zile za kimatibabu) pale zinapohitajika, hujikuta wanapoteza rasilimali zao kwa waganga wa kienyeji na wapiga ramli na bao. Imepelekea wengine kudharau matakatifu. Matokeo

yake ni kuvuruga mahusiano yao na Mungu na familia zao na majirani pamoja na kuharibu taratibu na mipango yao ya maisha.

Ni muhimu sana kusisitiza usomaji wa Neno la Mungu kuanzia katika familia. Familia inapokuwa shule ya sala, inawasaidia watoto kukua wakimjua Mungu na kushika tunu za kiutu.

3.2 Kimaadili na ukosefu wa tunu za kiutu

Tutambue kwamba, sote tumeumbwa kwa sura na mfano wa Mungu (Mwa.1:26-27). Kwa hiyo yatupasa kuwa na roho ya kutimiza wajibu wa kikristo wa kulinda hadhi ya utu wa kila mmoja na kushughulikia ustawi wa maisha ya wote. Inasikitisha kuona mienendo ya maisha yetu na hatua za kuboresha maisha yetu vinaenda kinyume na matashi ya Mwenyezi Mungu. Kutokana na kutokuwa na ufahamu wa kina wa Maandiko Matakatifu, wale wenye mamlaka / madaraka, wakati mwingine wanajikuta wa nafumbia macho maovu mengi yenye athari kubwa kwa familia zetu na jamii yetu.

Kinachoshuhudiwa kwa sasa ni mmomonyoko mkubwa wa maadili kwa rika zote lakini hasa kwa vijana. Hayo yanaonekana katika wengi wao kujitahidi kuondoa elimu ya uwepo wa Mungu ndani ya akili na mioyo ya watu, na hivi kuondoa uchaji wa Mungu. Kupenda kubadili jinsia, ushoga au ndoa za jinsia moja, au hata uzalishaji wa watoto kwenye maabara ni mifano wazi ya kuonesha mioyo isiyolijua Neno la Mungu na yenye kulikaidi. Endapo mambo kama hayo yatafundishwa shuleni au vyuoni, yatasababisha wengi kupotea.

Kwa ujumla, utu wetu umeshuka hadhi, na mwanadamu aliyeumbwa kwa sura na mfano wa Mungu haheshimiwi tena. Kanisa lifanye bidii ya kuongeza vipindi vya dini mashuleni na vyuoni ili kuokoa roho za wale wanaoingizwa kwenye upotofu huo kwa kukosa maarifa ya Neno la Mungu. Vikundi vya sala, pamoja na vyama vya kitume kama vile: Utoto Mtakatifu, TYCS, TMCS, VIWAWA, vitiliwe maanani sana, kwa ajili ya kumjenga na kumsaidia mtu kumjua, kumpenda na kumtumikia Mungu.

3.3 Kiutamaduni

Tamaduni potofu na madhara yake katika jamii zetu vimetokana na watu kukumbatia "tamaduni" za kigeni pasipo kujua madhara yake. Chanzo cha tatizo hili ni kutozijua tamaduni zetu sisi wenyewe. Mbaya zaidi hata wale wanaotakiwa kufundisha mila na desturi zilizo njema, hawafanyi hivyo siku hizi.

Kuna mambo mengi siku hizi yanayofikiriwa na jamii kuwa ni maendeleo lakini kwa kweli siyo hivyo. Kwa mfano: ndoa za mikataba, wazazi kutopenda kukaa nyumbani na watoto na kuwarithisha mila njema, uvaaji mbaya, kupiga picha muda wote kanisani badala ya kusali, kufuatilia tamthilia zikiukazo tamaduni njema za Kiafrika na mengine mengi yanayosababisha familia nyingi kusambaratika.

Tusisitize umuhimu wa kuwa katika familia. Zamani katika familia, kila mmoja alikuwa msimamizi wa mwingine; hivyo kusaidiana na kujiepusha na matatizo mengi. Mafundisho mema ya kikristo kama vile, familia inayosali pamoja hukaa pamoja ni muhimu sana kuyatekeleza.

3.4 Kiuchumi

Kwa kuumbwa kwa sura na mfano wa Mungu kunatufanya sote tuwe sawa kiutu. Ubinafsi, unaojidhihirisha katika vitendo kama vile: wizi, ukwepaji wa kulipa kodi halali, ulipishaji wa kodi zisizo halali na kwa manufaa binafsi, rushwa, ufisadi na magendo, vinaashiria kutoongozwa na Neno la Mungu. Tofauti kubwa baina ya walio nacho na wasio nacho, au matajiri wa kupindukia na maskini wa kupindukia ni matokeo yake.

Neno la Mungu lituongoze ili tuwe watu wa kiasi, haki na upendo. Bwana Yesu anatufundisha kupendana kama yeye alivyotupenda sisi (Yoh 13:34).

3.5 Kisiasa

Kutojua vizuri Neno la Mungu kwa wakati mwingine kumewapelekea watu (wanasiasa) kutafuta vyeo kwa njia ya rushwa, wizi wa kura na hata mahali pengine ya kutoa uhai wa watu wengine. Katika nchi nyingi za Kiafrika hili limekuwa "donda-ndugu" ambalo matokeo yake ni migogoro ya kivita na mapambano ya kiitikadi. Hii pia inatokana na tamaa mbaya za kisiasa ambazo mwelekeo wake ni kulinda maslahi binafsi na ulafi wa madaraka.

Mipasuko ya kisiasa ndani ya jamii huweza kutokea kwa sababu ya kikundi kimoja kujiona bora kuliko kingine, na wakati mwingine kujiona kiko juu ya sheria mbalimbali za nchi. Matokeo ya haya yote ni kufarakana kijamii, lawama zisizoisha na hivyo kuhatarisha amani na usalama wa jamii husika.

Tukumbuke kuwa Uongozi, madaraka au mamlaka yoyote ni dhamana kutoka kwa Mungu. Dhamana hii anapewa kiongozi kama mwakilishi wa Mungu katika kuongoza watu wa Mungu. Daima viongozi wafahamu kuwa wamepewa dhamana na Mungu kwa ajili ya wale wanaokabidhiwa (rej. Rum. 13:1).

Mafanikio ya kiongozi ni dhahiri pale anapomtegemea Mungu kabisa. Mtakatifu Paulo alisema kuwa, "sharti pawepo dua, sala, maombi na sala za shukrani kwa Mungu kwa ajili ya watu wote, kwa ajili ya wafalme na watu wote wenye mamlaka, ili tupate kuishi maisha ya utulivu na amani pamoja na uchaji wa Mungu na mwenendo mwema" (1Tim 2:1 – 2).

3.6 Uharibifu wa Mazingira

Mazingira ni mambo yote yanayomzunguka au yanayomzingira binadamu ambayo anaweza kuyatumia kwa faida au hata kwa hasara yake, kutegemea na jinsi anavyoyatumia vizuri au vibaya. Yote tuliyo nayo yatoka kwa Mungu hata sisi wenyewe (Mwa 1:28-31).

Kwa kushindwa kutii Neno la Mungu na kutolinda mazingira, tunajikuta tunafanya mambo ambayo yanaathiri uumbaji wa Mungu. Kwa mfano:

- Vitendo vinavyopelekea kuchafua hewa kwa njia ya moshi, vinavyoongeza joto, ni kama vile: milipuko ya mabomu, shughuli za viwandani, uchomaji wa mapori na miti ovyo. Matokeo yake ni maangamizi ya watu, wanyama na mimea, kutokana na kupanda kwa joto na kukosa hewa safi.

- Vitendo vinavyopelekea uchafuzi wa maji au ukaushwaji wa vyanzo vya maji ni kama vile: utupaji ovyo wa taka kwenye vyanzo vya maji na kufanya shughuli zingine za kibinadamu bila kujali kanuni za utunzaji wa vyanzo vya maji. Matokeo yake ni kukosa maji safi na salama kwa matumizi ya viumbe hai.

- Vitendo vya ukataji holela wa miti, kutopumzisha ardhi, idadi kubwa mno ya mifugo kwenye eneo moja, husababisha kutifuliwa kwa ardhi ambao utasababisha mmomonyoko wa udongo.

Ndiyo maana, kwa kuzingatia hayo, tunakumbushwa na Baba Mtakatifu Fransisko, kupitia barua *ensiklika* yake iitwayo, *Laudato Sí* – yenye kuhimiza kutunza mazingira yetu. Kwa maneno mengine, kwa kutii Neno la Mungu tu kutatuwezesha kutunza nyumba yetu ya asili – yaani ulimwengu aliouumba Mungu. Kuna madhara mengi yanayotupata pale tuachapo kulitii Neno la Mungu.

SURA YA NNE:

NINI KIFANYIKE?

4.1 Kiroho

Waamini wahimizwe na kuelekezwa na wachungaji kuyasoma Maandiko Matakatifu kila siku, kuyatafakari kwa faida ya roho zao wenyewe. Familia ni chanzo cha Jumuiya Ndogondogo za Kikristo na pia chanzo cha jumuia kubwa ya wakristo ambalo ndilo Kanisa. Kila mchungaji auzingatie wajibu huo wa kuliongoza kundi alilokabidhiwa katika kuyasoma Maandiko Matakatifu ambayo yatampa ufunuo wa ukweli kuhusu Mungu na ndiyo dira inayomwongoza na kumsaidia kila mkristo kumtambua Mwenyezi Mungu.

Pale ambapo muumini hajafanikiwa kuelewa vema ukweli ndani ya Maandiko Matakatifu, wajibu wa mchungaji ni kutumia vema nafasi hiyo kwa kumfafanulia vizuri ujumbe huo wa Habari Njema kwa watu wote, wajibu huo wa mchungaji ufanyike kwa makundi yote kadri ya uelewa wao, watoto, vijana, watu wazima na wazee. Waamini wote pia kwa ubatizo wao, wakiongozwa na Roho wa kweli, wanaalikwa kumfanya Mwenyezi Mungu afahamike kwa kila binadamu aliyeumbwa kwa mfano na sura ya Mungu mwenyewe. Mwaliko huu atautimiza kwa maneno na matendo yake ya kila siku.

Kuelewa kunahitajika kuwe na majiundo ya kiroho ya mtu binafsi na ya jumuiya. Majiundo haya hupelekea mtu kumcha Mungu ambako ndicho chanzo cha maarifa kwani "Kumcha Bwana ni chanzo cha maarifa, bali wapumbavu hudharau hekima na adabu" (Mit 1:7). Aidha, kila mmoja ana wajibu kiroho wa kuutafuta ukweli na kuuelewa. Ukweli

hupatikana kwa kuongozwa na walezi wetu wa kiroho wakiwemo maaskofu, mapadre, mashemasi, makatekista na wenye dhamana ya kutufundisha kiroho. Kama Kanisa hatuna budi kutambua kwamba anayetuongoza kuelewa kwenye ukweli wote ni Roho Mtakatifu, ambaye Kristo alituahidia akisema "Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote…" (Yoh 16:13).

Licha ya kuongozwa na viongozi wetu wa kiroho, Kanisa lina utajiri mkubwa wa wataalamu wanaoweza kutuongoza katika kuelewa Maandiko Matakatifu. Kanisa linatimiza wajibu huo kwa kutafsiri Biblia; kuchapisha Biblia kwa lugha nyepesi na inayoeleweka; kusomesha wataalamu wa Maandiko Matakatifu, mfano ni uwepo wa chuo cha kibiblia huko Roma (*Biblicum)*; kusomesha mapadre kwa ajili ya kuhubiri na kufafanua Biblia katika mahubiri na tafakari mbalimbali; na kupanga utaratibu wa kiliturujia ambapo watu hupata nafasi ya kutafakari Neno la Mungu katika mzunguko wa maadhimisho ya Ibada za Misa Takatifu kwa Miaka mitatu ya Kanisa, yaani A, B, C na mzunguko wa Mwaka I na Mwaka II. Haya yote yanatusaidia katika "kupenya kwa msingi wa kweli zilizofunuliwa."

Wakati huu wa Kwaresima ili kuweza kuwa tayari kuongozwa hatuna budi kuwa tayari kubadilika na kumrudia Mungu kwa njia ya toba na kuamini Neno kwa kuitikia mwaliko wa Kristo mwenyewe asemaye "Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia, tubuni, na kuiamini Injili" (Mk 1:15). Kutubu ni kutambua na kukiri njia zetu mbovu na kumwongokea Mungu; na kuamini Injili maana yake ni kukubali na kupokea huruma ya Mungu kwa njia ya Kristo ambaye yupo kati yetu. Hicho alichofanya yule Towashi

akakiri kutoelewa kwake, akakubali kuongozwa, akafanya toba na kuipokea Injili ndicho kilichomsaidia ayaelewe Maandiko Matakatifu.

Uelewa hutujengea nafasi ya kumjua Mungu, kushika maagizo yake ili tusiingie kwenye maangamizi. Watu wengi katika dunia hii huangamia kwa kukosa kumjua Mungu kupitia Maandiko Matakatifu ambapo huko tunapata njia iendayo uzimani. Kiimani na kiroho wadau wa uinjilishaji (agents of evangelization) tunaalikwa kuwauliza waamini wetu swali hili: **Je! Unaelewa?**

Swali la Filipo kwa Towashi akisema "Je! Unaelewa?," limejengeka kwenye juhudi au tamaa ya Towashi ya kumjua Mungu. Huyu hakuwa Myahudi. Alikuwa ni mshauri wa Malkia Kandake wa Ethiopia. Hivi uwezekano wa kuwa Muethiopia ni mkubwa. Hata hivyo hili halikumzuia kusoma Biblia ya Kiyahudi. Alisukumwa na utashi binafsi wa kumjua Mungu na matakatifu yake. Hii ndiyo tunaweza kuita tamaa ya kumjua Mungu ambayo ni msukumo wa ndani wa mtu binafsi katika kumjua Mungu na yale yote yaliyo yake. Msukumo huu ndiyo unaelekeza kupokea sakramenti mbalimbali mfano maungamo; pia kusoma maandiko mbalimbali yakiwemo Neno la Mungu, vitabu vya teolojia na vya maongozi ya kiroho, ngano za maisha ya watakafitu na kutafuta ushauri wa kiroho.

Jambo hili linatuingiza katika kile alichokuwa anaamini na kukiishi Mt. Anselm wa Kantabari (1033-1109). Teolojia yake ilijengeka katika falsafa inayojitokeza katika msemo ufuatao: *naamini ili nipate kuelewa*.[2] Wana heri

[2] *Credo ut intelligam*, Proslogion 1, msemo wa falsafa na teolojia ya Mt. Anselm wa Kantabari (1033-1109).

wanaoweza kuamini kabla ya kuelewa. Mtu akishaamini, taratibu anaanza kutafuta uelewa na ufahamu wa mambo anayoamini, kuamini kwanza na baadaye akatafuta kuelewa. Teolojia hii ilitawala hata sala zake, katika sala zake aliomba hivi:

> *Bwana Yesu Kristo,nakutafuta kwa kukutamani na nakutamani kwa kukutafuta, nakutafuta kwa kukupenda na nakupenda kwa kukutafuta*.

Imani ikiambatana na uelewa inakuwa bora sana. Mwandishi wa Waraka kwa Waebrania analiweka vizuri kwamba imani ni kuwa na uhakika wa yatarajiwayo na ushuhuda wa mambo yasiyoonekana (Ebr 11:1). Inahitaji ufunuo na mwanga wa Kimungu kuweza kujua yamhusuyo Mungu.

Baada ya kuona kuwa Towashi alikuwa anasoma kifungu hicho, kifungu kilichoendana sawia na yaliyompata Kristo, Filipo akamuuliza swali Towashi: *Je, yamekuelea haya unayosoma*? swali la Filipo ni la msingi. Tunaweza kuulizwa na mtu mwingine kama tunaelewa au sisi wenyewe tukajihoji juu ya uelewa wetu. Je! Tunaelewa? Tunaambiwa mambo mengi, tunaona mambo mengi na tunafundishwa mambo mengi. Tujiulize, je, tunaelewa?

Siyo Filipo tu aliyeuliza swali la namna hiyo. Bwana wetu Yesu Kristo alitoa mifano kadhaa juu ya ufalme wa mbingu, mfano mmojawapo ni ule wa mpanzi. Baadaye wanafunzi wake walimuuliza kwa nini unaongea nao kwa mifano, akafafanua ni kwa nini anatumia mifano katika kufundisha. Baadaye akawapa mifano mingine juu ya ufalme wa mbingu, na kisha akawauliza, *mmeelewa hayo*? (Mt 13:51).

Ingekuwa vigumu kwa Towashi kuelewa ujumbe wa kifungu alichokuwa anasoma mintarafu Yesu Kristo. Aliyotabiri nabii Isaya yalitimia baada ya miaka 450 baadaye katika nafsi ya Bwana wetu Yesu Kristo. Hii ni kuonesha kuwa sauti ya kinabii haifi. Aliyotabiri nabii huyo yanapata mwanga zaidi katika utume, mateso, kifo na kufufuka kwake Kristo. Na hayo ndiyo inabidi tutafakari katika kipindi hiki cha Kwaresima.

4.2 Kijamii

Jamii yetu kwa nyakati zetu, inajengwa na kundi kubwa lenye mchanganyiko wa watu mbalimbali. Ndani ya jamii kuna watu wanaomwamini Kristo, kuna wale wanaofuata mwelekeo wa upepo tu, wapo pia wanaoishi kwa mashaka kwa kuwa hawajaongozwa kumtambua Kristo na wapo ambao kwa hiari yao wameamua tu kukaa kando na wajibu wa kumwelewa Yesu Kristo na kumuishi. Ndani ya mchanganyiko kama huu mkristo anayetambua wajibu wake wa ubatizo anaweza kufahamu kazi kubwa iliyo mbele ya kila mbatizwa katika kuyaweka makundi yote kuwa kundi moja.

Kanisa na mitume wake wanaposhughulikia wale waliomo zizini tayari watambue pia kwamba wapo wengine ambao hawamo katika zizi na wanatakiwa wawemo. Kristo mwenyewe anasema, "Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta, na sauti yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja" (Yoh 10:16).

Dunia ya leo sauti nyingi za ulaghai zimeibuka, ni rahisi waamini kuyumbishwa na sauti hizo. Sauti nyingi

zinaposikika bila mpangilio, ni wajibu wa wachungaji na wote waliopewa mamlaka kuwaongoza waamini wao kwa sauti zenye mpangilio na sahihi katika njia ya wokovu.

Moja kati ya maeneo ambayo sauti zisizo na mpangilio zinasikika ni katika mitandao ya kijamii inayoifikia jamii kwa njia za utandawazi. Kijamii utandawazi umewafanya watu wengi, wakristo wakiwa miongoni mwao kuvutwa zaidi na malimwengu kuliko na mambo ya Kimungu. Matokeo ya kukosa mafundisho sahihi na ya kina ya Neno la Mungu ni kukithiri kwa vitendo vya mmomonyoko wa maadili katika jamii.

Jamii yetu inavutwa zaidi na mitandao ya kijamii ambapo huko tunapata vionjo na mafundisho ya kidunia zaidi kuliko mafundisho ya Kimungu. Tunapaswa kufundishwa na kuzingatia matumizi mazuri ya mitandao ya kijamii. Ni kazi ya Kanisa kuisaidia jamii kujua madhara hasi ya mitandao ya kijamii kama vile Filipo alivyomwongoza yule Towashi kuujua ukweli na kuuzingatia. Ni wajibu wa Kanisa kuongoza jamii kuelewa kile Kristo anachofundisha akisema "Mimi ndimi njia, kweli na uzima" (Yoh 14:6).

4.3 Kiuchumi

Uchumi wa Taifa hutegemea raslimali tulizojaliwa na Mwenyezi Mungu ili tuzizalishe na zitunufaishe kama Taifa. Kila binadamu kwa uwepo wake anayo haki na fursa ya kuelimishwa vema juu ya raslimali yoyote iliyomo ndani ya nchi yake na namna ya kuizalisha kihalali na kuitumia kwa utaratibu ulio sahihi bila kuwepo mwanya wowote wa ubadhirifu na unyonyaji. Mwenyezi Mungu ametupatia uwezo wa kuelewa katika viwango tofauti.

Kanisa linaamini na linawaalika walioelimika na kuelewa vema wawe msaada wa kwanza wa kuwaelimisha wengine kwa haki, ukweli na uwajibibikaji hasa inapohusu uchumi wa mtu mmoja mmoja na wa taifa kwa ujumla. Hili linaweza tu kufanyika kwa kuwa na hofu ya Mungu aliyetupatia raslimali zote kama zawadi kwetu. Ujumbe wetu wa Kwaresima wa mwaka huu unahimiza na kuwaalika wale wanaotumia nafasi zao, uelewa wao na mamlaka yao kujilimbikizia na kumiliki raslimali ambazo Mungu amezitoa kwa ajili ya watu wote badala yake wao wanazitumia kwa manufaa yao na familia zao. Shibe yao ya leo inayowaumiza walio wengi; na wao wenyewe inawafungulia mlango wa mateso wa maisha ya baadaye. Mfano wa maisha ya Lazaro na Tajiri (Lk 16:19-31) unatukumbusha jinsi gani utahukumiwa wewe unayejimilikisha uchumi wa Taifa kwa manufaa yako na familia yako bila kuwajali wengine walio maskini kama Lazaro.

Waraka wa Kwaresima Mwaka 2014 ("Ukweli utaweka huru": Yoh 8:32) ulisisitiza na kutukumbusha juu ya wajibu wetu wa kiuchumi wa kuhakikisha kwamba raslimali za Taifa zinawanufaisha watu wote. Waraka huo ulionya kwa kusema "Tumefikia mahali pa kuamini kwamba maendeleo yataletwa na kauli mbiu zinazobadilika badilika kila siku. Katika mazingira ya sasa, watu wachache, kwa sababu binafsi na kwa manufaa binafsi wanapotosha ukweli na kutafuta njia za kulinda maslahi yao kwa kutumia mifumo isiyokubalika, lakini inayosimikwa na kuhalalishwa ili kulinda maslahi binafsi. Hali hii inajidhihirisha kupitia matumizi mabaya ya madaraka, mikataba mibovu,

kupindisha sheria, kufumbia macho uhalifu... (Ujumbe wa Kwaresima, 2014, *"Ukweli utawaweka Huru"*,15).

Katika mazingira kama hayo Kanisa haliwezi kukaa pembeni na kutazama tu; linao wajibu wa kuangalia, kushauri, kuboresha na kuikosoa mienendo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa inayoweza kuhatarisha ustawi wa jamii nzima. Kanisa halina budi kuchukua nafasi yake kama ile ya Filipo aliyemsaidia Towashi kuelewa ukweli na hatimaye akaweza kuongoka.

4.4 Kisiasa

Kanisa linaamini kuwa kiongozi yeyote (halali) anatoka kwa Mungu (Rum 13:1b). Lakini namna ya kuongoza kwa uadilifu katika wajibu wake vinategemea uwezo wake na hofu ya Mungu aliyonayo. Siasa ni sauti ya watu kwa ajili ya watu wenyewe; bila shaka hawawezi kuitoa sauti ambayo wao wenyewe hawana. Ikiwa siasa inafikiriwa na kuchukuliwa katika maana ya "siasa ni viongozi" basi tutaendelea kuyashuhudia mengi yasiyo halali, haki wala adilifu.

Hayati Baba Mtakatifu Benedikto XVI aliona hatari ya viongozi wa kisiasa ambao pia hufanya maamuzi juu ya mwelekeo wa uchumi wa nchi zetu, na akaonya kwa kusema kwamba "Leo hii watu wengi wanaofanya maamuzi, wanasiasa na wachumi pia, wanadai kwamba wasidaiwe kitu na yeyote isipokuwa na wao wenyewe.

'Wanafikiri wao tu wana haki, na mara nyingi wana matatizo makubwa katika kuwajibika kwa ajili ya maendeleo kwa ujumla yanayowahusu wao wenyewe na wengine pia. Kwa sababu hiyo ni muhimu kuchochea tafakari mpya juu ya

namna haki zilivyosimikwa juu ya wajibu; bila kuwa hivyo, haki hizo zinageuzwa kuwa ubabe'" (*Africae Munus*: 82).

Kanisa lina wajibu wa kuwafanya wanatuongoza kuelewa kwamba kuongoza ni pamoja na uwakili wa kutunza vitu na mali walizokabidhiwa na Mungu. Ni kukubali kutumikia jamii katika wadhifa na uongozi kwa ngazi mbalimbali (rej. Mt 20:20-28). Aliye kiongozi hana budi kuwa mkweli, mnyofu na mwenye kuwajibika. Uongozi ni kudumisha na kuendeleza yaliyo mema na kukemea yaliyo maovu na kuyasahihisha. Licha ya wajibu huo mkubwa wa viongozi wa kisiasa, huenda hapa na pale na wao hawana budi kuongozwa ili watambue wajibu wao mkubwa kwa jamii.

Swali hili "Nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza?" (Mdo 8:31) liwape ufahamu viongozi wetu wa kisiasa kwamba yapo mambo mengi ambayo hawana budi kuelekezwa na kupata maarifa yake kutoka watu wa kada mbalimbali katika jamii wakiwemo viongozi wa dini na watu wenye taaluma nje ya siasa. Ili kufikia hapo, viongozi wetu hawana budi kuwa wachaji wa Mungu kwani "Kumcha Mungu ni chanzo cha hekima yote" (Mit:1:7). Nje ya uchaji wa Mungu, ipo hatari ya viongozi wetu wa kisiasa kujenga dharau, kiburi na kujenga tabia ya kujiona kwamba wao ni juu ya wote wanaowaongoza.

Tunakumbushwa daima kuwa cheo ni dhamana, na Yesu katika Maandiko Matakatifu amesema kuwa ukitaka kuwa mkubwa huna budi kuwa mtumishi (rej. Mt 20:26). Fadhila ya unyenyekevu ni ya muhimu kwetu viongozi na sisi sote kuwa tayari kupokea na kutenda kadiri ya maelekezo

ya Mungu na Roho Mtakatifu kupitia Neno la Mungu. Tukiwa na fadhila ya unyenyekevu tunaweza kuwa tayari kupokea maelekezo kutoka kwa wajumbe wa Mungu, hawa watatuongoza na kutuelewesha mpango wa Mungu kwetu.

HITIMISHO

Baada ya kusoma "Ujumbe huu wa Kwaresima" tunaalikwa sote kwa pamoja tuialike neema ya uongofu ituguse. Jitihada binafsi ya "**Towashi**" ya kusoma chuo cha nabii Isaya pamoja na kwamba alikuwa haelewi na jitihada ya Filipo kumfundisha na kumletea mwanga wa Kristo, kwa pamoja zilizaa matunda. Ujumbe huu wa Kwaresima unayaangazia matunda yaliyopatikana baada ya Towashi kuelewa, aidha matunda tegemewa baada ya sisi kuelewa. Ni matunda ya uongofu. Towashi alikubali kubatizwa. Ilikuwa ni ishara wazi kwamba alielewa na kukumbatia ukweli alioelezwa na Filipo. Hakulazimishwa bali ilitoka ndani mwake akisema, "*Tazama, maji haya: ni nini kinachonizuia nisibatizwe?*"; *naye Filipo akambatiza* (Mdo 8:36- 38). Uongofu na ubatizo huo ulileta furaha kwa Towashi.

Inawezekana wengine wanaosoma ujumbe wa Kwaresima hii hawajabatizwa! Baada ya kusoma ujumbe huu kwa nini wasiulize hilo "**ni** nini **kinachonizuia nisibatizwe**?" Ni kitu gani kinakuzuia usibatizwe, je ni uvivu, ni kutoelewa, ni kutojali au nini? Hata kwa wale tuliobatizwa bado kuna uwanja mpana wa kufanya mazuri zaidi katika Ukristo wetu. Kuna kurekebisha maisha binafsi ya kiroho; ndiyo maana vipindi vya kufanya toba vimewekwa na Kanisa. Kuna kurekebisha maisha ya wito na utume wetu kwa Mwenyezi Mungu na jirani. Kuna kurekebisha pia maisha ya familia zetu.

Neema zinazotokana na kipindi cha Kwaresima ziguse maisha yetu kwa namna ya pekee, yaani kurekebisha uelewa wa watu kuhusu imani, maadili yao, na kufanya

maazimio ya kuimarisha imani yetu hususan kuhudhuria Misa Takatifu, kupokea Sakramenti hasa Kitubio na Ekaristi Takatifu na juhudi za kutaka kujua zaidi juu ya imani yetu.

Wapendwa katika Kristu, tuiruhusu Kwaresima ya mwaka huu izae matunda ndani ya mioyo yetu, ndani ya familia zetu, ndani ya Kanisa letu na ndani ya Taifa letu. Hatimaye tunawatakieni matunda tele ya kipindi hiki cha Kwaresima, myasome na kuyaelewa vyema Maandiko Matakatifu; na mwishowe mjaliwe kushiriki furaha za Ufufuko wa Bwana wetu Yesu Kristo. *Na amani ya Kristo itawale mioyoni mwenu ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja tena iweni watu wa shukrani* (Wakolosai 3:15).

NI SISI MAASKOFU WENU

1. Mhashamu Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga, Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, Askofu Mkuu, Mbeya
2. Mhashamu Askofu Flavian Kassala, Makamu wa Rais, Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, Geita
3. Mwadhama Protase Kardinali Rugambwa, Tabora
4. Mhashamu Askofu Mkuu Yuda Thaddaeus Ruwa'ichi, Ofm Cap, Dar es Salaam
5. Mhashamu Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya, Ofm Cap, Dodoma
6. Mhashamu Askofu Mkuu Damian Dallu, Songea

7. Mhashamu Askofu Mkuu Isaac Amani, Arusha
8. Mhashamu Askofu Mkuu Renatus Nkwande, Mwanza
9. Mhashamu Askofu Tarcisius Ngalalekumtwa, Iringa
10. Mhashamu Askofu Agapiti Ndorobo, Mahenge
11. Mhashamu Askofu Augustino Shao,CSSp, Zanzibar
12. Mhashamu Askofu Severine NiweMugizi, Rulenge-Ngara
13. Mhashamu Askofu Ludovick Minde, ALCP/OSS, Moshi
14. Mhashamu Askofu Michael Msonganzila, Musoma
15. Mhashamu Askofu Almachius Rweyongeza, Kayanga
16. Mhashamu Askofu Rogath Kimaryo, CSSp Same
17. Mhashamu Askofu Eusebius Nzigilwa, Mpanda
18. Mhashamu Askofu Salutaris Libena, Ifakara
19. Mhashamu Askofu Bernadin Mfumbusa, Kondoa
20. Mhashamu Askofu John Ndimbo, Mbinga
21. Mhashamu Askofu Titus Mdoe, Mtwara
22. Mhashamu Askofu Joseph Mlola, ALCP/OSS, Kigoma

23. Mhashamu Askofu Prosper Lyimo, (Askofu Msaidizi), Arusha
24. Mhashamu Askofu Liberatus Sangu, Shinyanga
25. Mhashamu Askofu Edward Mapunda, Singida
26. Mhashamu Askofu Beatus Urassa, ALCP/OSS, Sumbawanga
27. Mhashamu Askofu Antony Lagwen, Mbulu
28. Mhashamu Askofu Filbert Mhasi, Tunduru Masasi
29. Mhashamu Askofu Simon Masondole, Bunda
30. Mhashamu Askofu Lazarus Msimbe, S.D.S, Morogoro
31. Mhashamu Askofu Stefano Musomba, OSA (Askofu Msaidizi Dar es Salaam)
32. Mhashamu Askofu Henry Mchamungu, (Askofu Msaidizi Dar es Salaam)
33. Mhashamu Askofu Wolfgang Pisa, Lindi
34. Mhashamu Askofu Christopher Ndizeye, Kahama
35. Mhashamu Askofu Thomas Kiangio, Tanga
36. Mhashamu Askofu Eusebio Kyando, Njombe
37. Mhashamu Askofu Jovitus Mwijage, Bukoba
38. Msgr. Vincent Mwagala (Askofu Mteule), Mafinga